**OFISI YA RAISI**

**TAWARA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA MTAMA**

**SHULE YA SEKONDARY MKOPWE**
**SLP. 235**
**MTAMA-LINDI**
**15.12.2020**

**KUMB N1 MTDC/MKSS/FMI/ADM/VOL1/20**

**JINA LA MWANAFUNZI :...........................................................................**

**SHULE ATOKAYO : ......................................................................................**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

1. Ninayo furaha kukuarifu na kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwwaka wa masomo unaoanza January ....................................
2. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/20........,unatakiwa kuripoti shuleni bila kukosa siku hiyo.Hatua za kisheria zitachukuliwa kwa atakayeshindwa kuripoti shuleni tarehe iliyotajwa hapo juu .
3. Masomo utakayojifunza ni Civics,History,Geography,English,Ekiswahili,Physics,Chemistry ,Biology na Basic Mathematics.
   Masomo yote yatafundishwa kwa lugha ya kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili .
4. Utakuwa unatumia lugha ya kiingereza muda wote uwapo hapo shuleni .
5. Nafasi hii uliyoipata ni muhimu sana kwako na Taifa kwa ujumla hivyo unatakiwa kuripoti shuleni bila kukosa na kwamba utatumia muda wako,akili zako na maarifa kwa kushirikiana na wanajumuiya wa shule hii ili kuwezesha kupata Elimu ,ambayo ndiyo kitu kikubwa na pekee kilichokuleta shuleni .
   Ni matumaini yangu kuwa utayatekeleza na kuzingatia mambo yote ili kurahisisha utoaji wa taaluma.
6. **TAFADHARI SOMA KWA MAKINI MAELEZO NA MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU .**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII :**

Attattaka
.................................................
ZAINABU S. MATAKA .

MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

1. SARE ZA SHULE

A: WASICHANA

- Sketi pea mbili ,rangi ya kijani ,aina ya kitambaa ni kitambaa kizito cha suti (Namba 1 )mshono wa linda box iwe ndefu.
- Blauzi iwe nusu kanzu mikono iwe nyeupe ,ndefu iliyobana mabega , ziwe pea mbili
- Shati nyeupe mikono mifupi,pea mbili kwa wale wasio vaa hijabu .
- Viatu vyeusi vya ngozi visigino vifupi pea mbili .
- Soksi nyeupe pea mbili.
- Leso (kitambaa cha mkononi )

B:WAVULANA:

- suruali pea mbili , rangi ya kaki,mshono wa celebration linda mbili upande wa kulia na upande wa kushoto na "MODO NI MARUFUKU'
- sharti nyeupe mikono mifupi pea mbili
- viatu nyeusi vya ngozi pea mbili
- soksi nyeupe pea mbili
- leso (kitambaa cha mkononi)
- mkanda mweusi wa ngozi usio na DSM ya madoido

ANGALIZO:Sare lazima ziwe za staha na heshima sawa na maadili ya kitanzania.Msichana sketi lazima iwe ndefu sio juu ya magoti na mvulana suruali yake isiwe modo na sehemu ya chini lazima ifunike visigino vya viatu vyake ikiwa imekaa kisawa sawa kiunoni mwake visigino vya viatu vyake ikiwa imekaa kisawasawa kiunoni mwake .

TAFADHARI :MZAZI SIMAMIA USHONAJI WA SARE ZA SHULE ZA MTOTO.

2:VIFAA VYA TAALUMA :

- daftari kubwa (counter books )10
- peni ,penseli,rula na vifutio
- mkebe 1.
- Rim moja ya karatasi
- Dictionary ya kiingereza
- Begi la kuhifadhia /kubeba vifaa hivyo
- Faili moja la plastistic au Tsh 2000/=
- Passport size tatu

**3:SAMANI :**

**MWANAFUNZI ANATAKIWA KUJA NA KITI CHAKE CHA KUKALIA :KITI KINAWEZA KUWA CHA PLASTIKI AU MBAO**

**4:VIFAA VYA MICHEZO(WASICHANA NA WAVULANA )**

- Viatu aina ya Raba
- Trakisuti au Bukta rangi ya blue
- Fulana ya shule inapatikana shuleni kwa shilingi elfu kumi na mbili (12000)

**5:VIFAA VYA USAFI NA ELIMU YA KUJITEGEMEA**

**WASICHANA**

- ➢ Jembe aina ya ngwamba lenye mpini
- ➢ Slesha (kwanja/fyekeo )
- ➢ Ndoo ndogo ya plastiki (kisado )
- ➢ Fagio la chelewa

**WAVULANA**

- ➢ Embe aina ya ngwamba
- ➢ Panga
- ➢ Ndoo ndogo ya plastic(kisado)
- ➢ Fagio la chelewa

**6:MICHANGO:**

- Fedha Tshs=5000/=(Elfu tano tu )kwa ajili ya mchango wa photocopy machine
- Tofali 4 (nne) na tshs = 2000 /=(elfumbili tu ) kwa ajili ya mchango wa ujenzi wa hosteli.

## FORM NO 2

## 3;0 SHERIA, TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE YA SEKONDARI [redacted]

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheia ya Elimu na25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na 10 ya mwaka 1995.

Aidha inazingitatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu sayansi, Tekinolojia na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu ya usimamizi na uendeshaji wa Elimu,

Unatakiwa kusoma kwa makini na kuzingatia mambo yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni.

i. Heshima kwa viongozi, wazazi ,wafanyakazi, wanafunzi wenginena jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
ii. Mahudhurio katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (remidial and evening preparation)
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyinginezo utakazopewa
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya uwepo wa ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
vii. Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule na
ix. Kutunza mali za Umma

## 3;1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

1. Uasherati, ubakaji na ushoga
2. Ulevi, uvutaji wa bangi na matumizi ya madawa ya kulevya
3. Kupiga au kupigana
4. Kuharibu makusudi mali ya shule/umma
5. Kudharau Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa, Picha za Viongozi waTaifa , Nembo ya Taifa na Fedha za Taifa
6. Kuoa au kuolewa
7. Kupata au kusababisha mimba na kutoa mimba ndani au nje ya shule
8. Kugoma / kuchochea /kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu na mali zao
9. Kukataa adhabu
10. Wizi
11. Kunyanyasa wanafunzi wenzake
12. Kumiliki au kutumia simu shuleni
13. Kutoka nje ya shule bila kibali maalumu cha mwalimu wa zamu au mkuu wa shule

## MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUADHIBIWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

1. Kutosimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita kuingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano na mahali pengine popote
2. Kuvaa viatu vyovyote vya mikanda vikiwemo kandambili, ndala bajaji n.k shuleni
3. Kutumia lugha chafu dhidi ya wanafunzi wenzake , kwa walimu au mtu mwingine yeyote.
4. Kutovaa sare sahihi mf. Modal trousers
5. Kutowaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni kama walezi wake
6. Kutoonyesha dhamira ya kushirikiana kazi kwani kazi ni kielelezo cha utu
7. Kutoheshimu au kutothamini kazi za aina zote zinazotolewa na uongozi wa shule
8. Uvutaji sigara
9. Kufuga ndevu
10. Kuvaa mavazi yasiyokuwa na heshima
11. Kutotii kengele au kushindwa kuitikia mwito wa kiongozi aliyemwita
12. Kutoheshimu picha za viongozi wa serikari, nembo ya taifa , wimbo wa taifa na fedha za taifa
13. Kutosimama katika utaratibu maalumu wakati wa kupokea huduma
14. Kutoheshimu na kutokubali tofauti za kisiasa, kidini na kiutamaduni
15. Kutohudhuria vipindi vy madarasani kwa muda wote wa masomo
16. Kutohudhuria kazi zote za mikono , mikutano yote ya shule, ukaguzi na usafi na kupandisha bendera ya taifa.
17. Kushindwa kuthamini muda
18. Kutowahi katika kazi zote kama zilivyopangwa ukiwemo wito wa dharura
19. **Kutovaa sare za shule katika sehemu zifuatazo**
    a. Darasani
    b. Shughuli za kishule nje ya shule
    c. Mhadhara wa shule (school baraza)
    d. Kwenda kutibiwa hospitali
    e. Kwenye maandamano yasiyo rasmi
    f. Anaposafiri kwenda na kurudi likizo
20. Kuvaa kofia, viatu vya gorofa na kandambili na mapambo yoyote, kama pete, mkufu, rozari,takibiri, heleni, na baangili
21. Kutokuwa msafi wa mwili na nguo
22. Kutoheshimu mipaka ya shule
23. **Marufuku kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa**
    a. Ofisi ya walimu (staffroom)
    b. Ofisi za shule
    c. Maabara
    d. Jikoni
    e. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu
24. **Sehemu zifuatazo ni marufuku kabisa kutembelea**
    a. Vilabu vya pombe
    b. Kumbi/nyumba za starehe
    c. Nyumba za kufikia wageni (Guest House)
    d. Pull table
    e. Kumbi za video
    f. Maeneo ya kamali

FORM NO 3

MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATION TRAINING

~~CHIUTA~~ MKOPWE SECONDARY SCHOOL
P.O BOX ~~114~~ 235
MTAMA- LINDI

REF. NO.........................................................

THE MEDICAL OFFICE,
...................................................................................

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF**

MR/MS........................................................................................................
...

Please examine the above named pupil and give us report regarding his/her suitability for secondary school studies.

1. Pupil's full name........................................................................
2. Blood..........................................................................................
3. Stool...........................................................................................
4. T.B Test.....................................................................................
5. Syphilis test...............................................................................
6. Urine examination.......................................................................
7. Eye test.......................................................................................
8. Chest...........................................................................................
9. Ears...........................................................................................
10. Spleen.........................................................................................
11. Abdomen.....................................................................................
12. Pregnancy (GIRLS ONLY)........................................................

I certify that the above pupil is suitable/unsuitable for studies. Give reasons..........................................................................................................
.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
.........................................................................................................................

Name of medical officer..................Signature...........Date.............Stamp...............

..........................................

MS. ZS MATAKA

HEADMISTRESS

MA... WASHULE
...LI Y YA SEKONDARI CHIUTA
LIND (V)